*Kioo cha Lugha, Juz. 21(1), 169-192*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v21i1.10

# Nyimbo za Jando za Jamii ya Wagogo na Maudhui yake

*Rose J. Mbijima*[1]

## Ikisiri

Nyimbo za jando ni utanzu mmojawapo wa fasihi simulizi ya makabila mengi. Kabla ya ujio wa wageni asasi ya jando ilitazamwa kama chombo cha ujamiishaji na uhifadhi wa hekima na falsafa za jamii. Kupitia nyimbo za jando mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa vijana na jamii kwa ujumla. Makala hii imechunguza nyimbo za jando za jamii ya Wagogo na kubainisha maudhui yanayojitokeza katika nyimbo hizo. Nadharia ya Sosholojia ya Fasii iliyotumika katika utafiti huu imetuwezesha kuzikusanya na kuzichambua data za awali na za upili. Data za awali zimekusanywa katika tarafa ya Kongwa mkoani Dodoma kwa kutumia mbinu za mahojiano na ushuhudia. Data za upili zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya upitiaji nyaraka uliofanywa kwenye maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Utafiti huu umebaini kuwa nyimbo za jando za jamii ya Wagogo zina maudhui mbalimbali na ya msingi yakiwamo; umuhimu wa tohara kwa vijana, kuwaandaa vijana kumudu majukumu ya utu uzima, ujamiishaji na uadilishaji vijana. Mengine ni ukarimu, umoja na ushirikiano katika jamii, umuhimu wa kudumisha mila, desturi na utamaduni wa jamii na masuala ya kijinsia.

## 1.0 Utangulizi

Utafiti wa tanzu na vipera vya fasihi simulizi, zikiwamo nyimbo, umefanywa na wanazuoni na wataalamu wengi kama vile Finnegan (2012), Mulokozi (1983) na Madumulla (1995). Tafiti zao zimebainisha wazi kwamba jamii anuai za Kiafrika zina utajiri mkubwa uliomo katika fasihi simulizi. Hata hivyo, uchunguzi wa nyimbo hususani za jando haujafanywa vya kutosha. Mulokozi (2011) akibainisha matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi, pamoja na mambo mengi anasema kuwa, tatizo jingine ni lile la watafiti waliotangulia kutozipa umuhimu nyimbo ziimbwazo katika kumbi. Ni watafiti wachache sana walioona umuhimu wa kuzirekodi na kuzijadili nyimbo za

[1] Mhadhiri, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: rosembijima2019@gmail.com

unyagoni na jandoni. Kwa msingi huo, makala hii inachunguza nyimbo za jando za kabila la Wagogo na kuibua maudhui anuai katika nyimbo hizo.

Kumbi ni asasi ya kimiviga, yaani matendo ya kimila ambayo hupatikana katika jamii nyingi za Tanzania. Kumbi ni asasi ya ujamiishaji, huwaingiza vijana katika jamii zao, huwafanya wawe jamii halisi kwa mawazo, hisia, mwonekano na matendo. Istilahi ya kumbi inajumuisha jando kwa wavulana, na unyago kwa wasichana (Nassoro, 2011). Unyago unahusu hatua kubwa tatu; kumtoa rasmi msichana kutoka kundi la watoto, kumfundisha yale yanayohusika na utu uzima na kumwingiza rasmi katika kundi la watu wazima (Mhando na Balisidya, 1976).

## 2.0 Tafiti kuhusu Nyimbo za Jando na Jando kwa Jumla

Sehemu hii inapitia mawazo mbalimbali ya wataalamu walioandika kuhusu jando kama kipengele kimojawapo cha mila na destuiri za Wafrika. Vilevile, maandiko yanayofafanua kuhusu nyimbo yamepitiwa. Kiango (1995) anaeleza kuwa jando ni hatua ya malezi ya kijana katika jamii nyingi za Kiafrika. Anaendelea kusema kwamba, katika jando vijana hufundishwa mambo kama vile ujinsia, uzazi, malezi na uvumilivu. Naye Kigume (2011:120) anaeleza kwamba jando ni kipengele cha mila na desturi ambacho ni muhimu katika kutoa mafunzo yanayofaa kuendeleza maadili ya nchi wakati huu ambapo taifa linajaribu kujenga utamaduni wa taifa zima unaotokana na mila na desturi za watu wake. Kigume anaendelea kusema kwamba, jando ni sanaa kwa kuwa inahusisha matendo mbalimbali yanayoambatana na uchezaji wa viungo vya mwili, uimbaji wa nyimbo, kutingisha mabega, matumizi ya taswira na mafumbo. Pia, kuna ubunifu katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii. Nyimbo nyingi zinazoimbwa zinabeba ujumbe kwa njia ya kisanaa (Mlama, 1981; Kigume, 2011). Hivyo, jando na unyago hutumia sana fani za kifasihi ili kufanikisha malengo yake. Mulokozi (2011:12) anadai kwamba kwa upande wa fasihi simulizi, tanzu za methali, vitendawili, vitanzandimi, hadithi ushairi au nyimbo za maghani na maigizo hutumika zaidi. Mdachi (1991) akinukuliwa na Kigume (2011: 118) anaeleza kwamba “pamoja na sherehe zinazofanywa baada ya vijana kutahiriwa wazee, hufurahia vijana wao kutoka katika hali ya utoto na kuingia kwenye hali ya ujana. Hivyo, jando ni asasi muhimu katika jamii ambapo mafunzo mbalimbali hutolewa.”

Mnyampala (1954) akiandika kuhusu jando la jamii ya Wagogo anasema kuwa kijana arudipo toka jandoni anakuwa na akili timamu. Katika jamii hiyo mtoto anaposhindwa kushika mafunzo yanayotolewa jandoni mizimu inakuwa imedharauliwa na hivyo hukasirika. Simeon (1977) anaweka uzito kwenye maelezo ya Mnyampala (1954) kwa kusema kwamba jando ni sehemu ya fasihi simulizi ambayo nyimbo zake zina nafasi ya kutoa elimu kwa jamii ili kuondokana na ujinga kwa lengo la kuifanya jamii hiyo kuwa na mwelekeo mzuri na kuzingatia

maadili mema. Mafundisho ya jando humwandaa kijana wa kiume kuweza kuchukua majukumu ya jamii husika (Kigume, 2011:114).

Simeon (1977) anaeleza umuhimu wa jando katika jamii ya Wapare kuwa ni kufunza mambo ya utu uzima kama vile elimu, uzazi na ngoma ya kuchezea msituni. Kwa jumla, jando huwaandaa watoto kuingia utu uzima. Pia, hufunzwa namna ya kumudu majukumu ya utu uzima katika familia zao watakapooa au kuolewa. Isitoshe, vijana wawapo jandoni huelezwa kwa nini matumbo ya mama zao huwa makubwa, yaani hufunzwa namna mimba inavyotungwa. Kutokana na umuhimu wa mafunzo yanayotolewa jandoni, wazazi waliojaribu kuwaficha watoto wao walichekwa. Pia, kijana asiyepitia jando hata kama atakuwa na umri mkubwa kiasi gani, alidharauliwa na kuonekana kuwa bado hajakua.

Kwa upande wa Kiango (1995) akinukuliwa na Kigume (2011:119), anaeleza kuwa jando ni chuo muhimu cha mafunzo ya maisha ya Pwani ya Kusini ambayo humtoa mtoto kutoka katika usungo na kumtia uromboni. Katika jando watoto hufundishwa mambo ya jinsia, uzazi, ulezi na uvumilivu. Naye Taban (1972) anasema kuwa umuhimu wa kijana kupelekwa jandoni kutahiriwa pindi anapofikia karibu na utu uzima ni kumwandaa katika maisha ya kiutu uzima. Kwa jumla, kabla ya kuja kwa ukoloni, jando lilishika nafasi ya asasi za elimu kama shule na vyuo tulivyo navyo sasa. Jando lilikuwa linawatayarisha vijana kubeba majukumu mbalimbali ambayo watu wazima walishughulikia na hatimaye kuwakabidhi vijana hao. Vijana hawakuweza kukabidhiwa majukumu hayo bila kupitia hatua hii muhimu ya jando.

Naye Mulokozi (2011: 2) anaeleza kwamba kumbi ni asasi ya kimiviga yaani matendo ya kimila ambayo hupatikana katika jamii nyingi za Tanzania. Ni asasi ya ujamiishaji ambayo huwaingiza vijana katika jamii zao, huwafanya wawe wanajamii halisi kwa mawazo, hisia, mwonekano na matendo.” Istilahi ya kumbi ambayo hujumuisha dhana ya unyago (wasichana) na jando (wavulana), ni asasi mahususi ambayo huambatana na miviga na fasihi. Mulokozi (2011) akijadili kuhusu uhusiano wa kumbi na fasihi, anaangalia jinsi nyimbo za kumbini zinavyoakisi itikadi, mila na matarajio ya jamii au makundi ya kijamii katika kuwaandaa vijana kuwa watu wazima.

Kwa upande mwingine, kuna maandiko yanayofafanua kuhusu nyimbo, ambapo Kezilahabi (1980) akichunguza nyimbo za Wanyamwezi, Wakerewe, Wahaya na Wajita, anasema, “Nyimbo hubeba utamaduni lakini utamaduni wa jamii hubadilika sambamba na mabadiliko hayo.” Aidha, Mazingwa, (1991:32) anafasili nyimbo kuwa ni, “Utanzu muhimu katika makabila mbalimbali ya kibantu, wenye kupitisha mafunzo mbalimbali kwa jamii.” Kupitia maudhui ya nyimbo hizo, mafunzo ya aina mbalimbali hutolewa kulinga na matakwa na falsafa ya jamii. Isitoshe, Msokile (1992) anasema kuwa nyimbo ni aina ya ushairi wenye kuimbwa na kutumia ngoma au wakati mwingine kufuatiwa na mapigo ya kishairi.

Nyimbo nyingi hujikita katika kuonesha mambo mbalimbli yaliyomo katika jamii kama vile umoja, ushirikiano, ukandamizajij, usaliti na ubadhilifu. Naye Wamitila (2003) anasema kwamba wimbo ni kazi ya kisanaa ambayo hutoa wazo au tukio kwa namna inayovuta hisia kutokana na mpangilio maalumu wa maneno yaliyoteuliwa, kauli za mkato na picha.

Vilevile, Ngure (2003: 72) anafasili wimbo kuwa ni utungo ulio na mdundo na mahadhi na unaoweza kuimbika. Anasema kuwa nyimbo ni maarufu sana katika jamii nyingi za Afrika na kwamba shughuli nyingi za Waafrika zinaandamana na nyimbo, dansi na ngoma. Naye Kauti (2013:13) anasema kuwa nyimbo ni aina ya ushairi uliotiwa sauti na uliokusudiwa kuimbwa na kuleta maana na ujumbe kwa jamii. Nyimbo nyingi huwa na kibwagizo ambacho ni kiitikio kwa watu wote wanaoshiriki kuimba.

Kwa jumla, kuna nyimbo za aina mbalimbali kutegemeana na dhima na muktadha wa jamii husika. Makala hii inajadili utanzu mmoja wapo wa nyimbo kama ulivyoanishwa na (Mulokozi, 1989; 2017). Utanzu wa nyiso ambao una vipera viwili, nyiso za jando na nyiso za unyago, Makala kwa hiyo, yanashughulikia nyiso za jando za jamii ya Wagogo, kwa kuyabainisha maudhui yanazoibuliwa katika nyimbo hizo.

**3.0 Data za Utafiti**

Utafiti huu umefanyika Mkoani Dodoma hususani katika Wilaya ya Kongwa, Tarafa ya Kongwa, Vijiji vya Mlanga, Mnyakongo, Kongwamaji na Viganga. Hata hivyo, Data za utafiti huu zingeweza kukusanywa kutoka wilaya au tarafa yoyote ya mkoa wa Dodoma. Kwa kuwa haikuwa rahisi kufanya utafiti katika mkoa mzima, vijiji vichache vilichaguliwa kinasibu ili kuwakilisha mkoa tajwa. Utafiti umetumia data za aina mbili, za msingi na za upili. Data za msingi zilipatikana kwa kutumia mbinu ya mahojiano na ushuhudiaji. Mahojiano yaliwahusisha wazee, ngariba, wanaume, wanawake na vijana waliotahiriwa kutoka vijiji tajwa. Makundi haya ya watafitiwa yamechaguliwa kutokana na uzoefu wao katika masuala ya jando. Wazee walihusishwa kwa kuwa ndio wanaojua mila na desturi za jamii. Hata hivyo, siyo wazee wote ni ngariba, hivyo, ilikuwa ni muhimu kuwahoji ngariba ili kupata data ambayo hatungeweza kuipata kwa wazee. Vilevile, wanaume ndio hushiriki katika kuwatunza na kuwahudumia vijana wakati wote wawapo jandoni, hivyo, tuliwahoji ili kupata data tulizozihitaji. Kwa upande wa wanawake, wao walihojiwa kwa kuwa kwa kawaida hushiriki kikamilifu kuziimba nyimbo za jando wakati wa usiku, wakati vijana wanatembelea nyumba na siku ya sherehe ya kuwatoa vijana jandoni bada ya kuhitimu mafunzo yao. Aidha, mbinu ya ushuhudiaji imetumika kukusanya orodha ya nyimbo za jando ambazo zimetumika katika utafiti huu kama data za msingi.

Kwa upande mwingine, data za upili zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya upitiaji nyaraka maktabani katika maktaba ya Chuo Kikuu Dar es Salaam na Makavazi ya TATAKI. Nyaraka zilizopitiwa ni zile zinazohusu nyimbo za jando na mila na desturi za jamii ya Wagogo. Aidha, nyaraka zinazohusu fasihi simulizi kwa jumla pia zilipitiwa kwa uelewa mpana zaidi wa mada ya makala haya. Uteuzi wa maktaba tajwa umetokana na ukweli kwamba maktaba hizi zimesheheni data zilizokuwa zinahitajika kukamilisha uandishi wa makala haya.

**4.0 Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi**

Kwa mujibu wa Coser (1963), Leenhardt (1967) na Goldmann (1967) mwasisi wa Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ni Georg Lukacs (1885-1971). Sosholojia ya Fasihi ni nadharia inayochunguza mahusiano kati ya sanaa, umma na muundo wa kijamii. Nadharia hii hukusudia kueleza sababu zinazochangia kuzuka kwa kazi ya sanaa iliyo na umbo la kijamii na namna fikra za ubunifu za mwanafasihi zinavyoongozwa na mila, desturi na mpangilio wa jamii inayohusika (Coser, 1963). Wahakiki wa Kisosholojia huzingatia jinsi kazi ya fasihi inavyoathiriwa na mazingira na kushikilia kuwa kazi ya kifasihi imedhibitiwa na muundo wa jamii (Wamitila (2003:204).

Aidha, nadharia hii inachukulia kuwa kazi za kifasihi ni nakala ya tabia, mila na desturi na kiwakilishi halisi cha maisha ya jamii fulani wakati huohuo (Njogu & Chimerah, 1999). Hivyo, nadharia hii inayatazama mazingira ya asili ya jamii kwamba ndiyo huamua namna kazi ya kifasihi inavyotakiwa kuwa. Kwa hiyo, msanii wa kazi ya fasihi hawezi kukwepa athari za jamii katika kazi yake kwani fasihi ni zao mahususi la jamii yake (Sarup, 1989; na Booker, 1996). Lukacs (1962) akizungumzia uhusiano uliopo kati ya fasihi na jamii, anasema kuwa fasihi, nyimbo za jando zikiwemo, husawiri maisha ya jamii kulingana na wakati na kwa kuzingatia mabadiliko ya kihistoria ya jamii. Hivyo, tunaingalia kazi ya fasihi kuwa ni zao la jamii na inaweza kueleza historia ya jamii. Katika msingi huo, Sosholojia ya Fasihi humzingatia binadamu kama uti wa mgongo wa ulimwengu huu na sanaa kwa jumla (Caleb, 2013). Wajibu wa mhakiki wa kisosholojia ni kuiweka kazi ya kifasihi katika ulimwengu wa kijamii na kueleza uhusiano uliopo kati ya kazi hiyo ya fasihi na jamii (Msokile, 1992; Welleck & Warren, 1949; Coser, 1963; Caleb, 2013).

Katika utafiti huu, Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi imetuongoza katika kuorodhesha nyimbo za jando ambazo ni nakala ya tabia, mila, desturi na kiwakilishi halisi cha maisha ya jamii tajwa. Aidha, nadharia hii imetuongoza kuzichambua nyimbo za jando ambazo ni zao mahususi la jamii ya Wagogo. Pia, nadharia imetuwezesha kuonesha jinsi nyimbo ambavyo nyimbo za jando za Wagogo haziwezi kukwepa athari za jamii husika kwa kuyabainisha maudhui katika nyimbo hizo.

## 5.0 Maudhui Yanayoibuliwa katika Nyimbo za Jando za Jamii ya Wagogo

Kutokana na tamaduni za jamii ya Wagogo, vijana wanapopelekwa jandoni wanapitia vipindi mbalimbali toka siku ya kwanza wanapotahiriwa hadi siku wanapofanyiwa sherehe ya kutolewa jandoni. Kwa kawaida kipindi cha kukaa jandoni hutegemea maendeleo ya kiafya ya vijana waliotahiri lakini mara nyingi hakizidi wiki tano. Kipindi ambapo vijana hukaa jandoni hususani kuanzia wiki ya pili au ya tatu ambapo vijana huwa wameshaanza kupona vidonda, huambatana na uimbaji wa nyimbo ambazo huitwa nyimbo za jando. Nyimbo hizo hubeba au kuibua maudhui tofautitofauti kutegemea na wahusika, mahali na wakati zinapoimbwa. Katika sehemu inayofuata tumebainisha maudhui yanayobebwa katika nyimbo za jando za jamii ya Wagogo.

### 5.1 Umuhimu wa Tohara kwa Vijana

Nyimbo za jando za jamii ya Wagogo zimebeba maudhui yanayoonesha umuhimu wa tohara kwa vijana. Maudhui haya hueleza umuhimu wa kutahiri kuwa ni pamoja na kukipa kiungo cha mwanamume mwonekano mzuri na kudumisha usafi. Kwa mfano, katika wimbo unaoitwa *Mpela wali mubi* maudhui haya yanajidhihirisha, wimbo unasema:

Kiongozi: *Mpela wali mubi nyeee x 2*
*Sese causesa ne mbazo,*

Tafsiri

Kiongozi: *Mbuyu ulikuwa mbaya weee x 2*
*Sisi ndio tuliouchonga kwa kisu*

Wimbo huu unasema kuwa mbuyu ambao una maana ya kiungo cha kiume, ulikuwa mbaya kabla ya kutahiriwa lakini sasa umechongwa umekuwa mzuri. Aidha, maudhui kama haya yanajitokeza kwenye wimbo unaoitwa *Cibandya* ambao unasema:

Kiongozi: *Cibandya,*
Wote: *Cahimbahimba calemwa x 4*

Tafsiri

Kiongozi: *Kipanya,*
Wote: *Kilichimbachimba kikashindwa x 4*

Maudhui ya wimbo huu ni kuonesha madhara ya kutokutahiriwa ambayo ni kushindwa kufanya tendo la ndoa. Kipanya kilichoshindwa kuchimba na kuingia kwenye shimo maana yake kiungo cha kiume ambacho hakijatahiriwa kushindwa kufanya tendo la ndoa.

Wimbo mwingine ni ule unaoitwa *"Nye Wadodo Mwaliye ci*? Wimbo unauliza:

| | |
|---|---|
| Kiongozi*:* | *Nye wadodo mwaliye cii?* |
| Wote: | *Caliye itanga x 2* |
| Wote*:* | *Itanga itanga itanga itanga* |
| | *Kuli yaya gwee nalimanye nikale* x 2 |
| | *Itanga ikali mnooo* |

Tafsiri

| | |
|---|---|
| Kiongozi*:* | *Nyie watoto mmekula nini?* |
| Wote: | *Tumekula tango x 2* |
| Wote*:* | *Tango, tango, tango, tango* |
| | *Mama yangu wee ningejua nisingekwenda* x 2 |
| | *Tango kali mno* |

Mwimbaji anawauliza vijana wamekula nini, nao wanajibu wamekula tango chungu wangejua wasingekula. Ugogoni kuna aina mbili za matango; yanayofaa kuliwa na yasiyofaa kwa kuwa ni machungu. Vijana kwa hiyo, wanafananisha maumivu ya kutahiriwa na uchungu wa matango hayo. Pamoja na uchungu huo, wazazi wanawaruhusu watoto wao kufanyiwa tohara, hii ni kutokana na umuhimu wa tohara kwa vijana. "*Usungu wo tamwa gwe Mauya"* yaani uchungu unauma wee Mauya (jina la mtu), ni wimbo mwingine unashadidia kuhusu uchungu wa kutahiriwa. Isitoshe, umuhimu wa tohara unaelezwa kupitia wimbo wa "*Dimkakame*" ambapo waimbaji wanashangilia kuwa ngozi iliyokakamaa na mbaya imechinjwa na shoka. Wimbo unasema:

| | |
|---|---|
| Kiongozi: | *Dimkakame* |
| Wote: | *Dyaulagwa na nhemo x 4* |

Tafsiri:

| | |
|---|---|
| Kiongozi: | *Lingozi lililokakamaa* |
| Wote: | *Limechinjwa na shoka x 4* |

Wimbo huu unaeleza umuhimu wa kuiondoa ngozi ili kudumisha usafi na kuwaepushia vijana magonjwa. Aidha, wimbo wa "*Citunda cha Maombo kucanhya capiye moto"* yaani kamlima ka Maombo (jina la mahali) kileleni kinawaka moto, unasifia kiungo cha mwanamume kilichotahiriwa kuwa kinapendeza kama kamlima kanakowaka moto kileleni. Mjadala huu wa umuhimu wa tohara kwa vijana unashabihiana na mawazo ya wanasosholojia ambao wanaeleza jinsi nguvu za kijamii zinavyohusiana na nguvu za kisanaa (Narizvi, 1982). Wanaona kuwa kazi ya fasihi inadhibitiwa na miundo iliyopo katika jamii kwa kuangalia uhusiano wa wanajamii katika mienendo yao ya kila siku. Nyimbo

za jando za Wagogo kwa hiyo, zimetazamwa kama usawiri mkamilifu ambao huyasawiri maisha kwa undani na huyachunguza kwa mtazamo mpana.

**5.2 Kuwaandaa Vijana Kumudu Majukumu ya Utu Uzima**

Mafundisho ya jando humwandaa kijana wa kiume kuweza kuchukua majukumu ya jamii husika (Kigume 2011). Nyimbo za jando za jamii ya Wagogo zimesheheni maudhui yanayowaandaa vijana kwa ajili ya majukumu ya utu uzima. Kupitia nyimbo hizi, vijana hufunzwa namna ya kumudu majukumu ya utu uzima katika familia zao watakapooa. Mafunzo haya yalitolewa kwa njia ya nyimbo zinazoimbwa vijana wawapo jandoni. Tuone mifano ya nyimbo za jando za Wagogo zinazozibeba maudhui ya tajwa.

Kwanza, kuna wimbo unaitwa *Kono ndawile simbuyaga ndabuce* ambao umebeba maudhui kuhusu umuhimu wa mwanamume kutosheka wakati wa tendo la ndoa. Wimbo unawafundisha vijana umuhimu wa kufanya tendo la ndoa kwa ustadi na ukamilifu ili kukata kiu yote. Wimbo unasema:

Kiongozi: *Kono ndawile simbuyaga ndabuce,*
Wote: *Kono ndawile simbuyaga ndabuce x 2.*

Tafsiri

*Kiongozi:* *Nilikotoka huwa sirudi nikiwa njaa,*
*Wote:* *Nilikotoka huwa sirudi nikiwa njaa x 2.*

Aidha, wimbo unaojulikana kama *Mwana mikula* ambao unaona kuwa watoto na vijana wenye tabia ya kuamka mapema na kwenda kwenye nyumba au chumba cha wazazi kuwa ni watovu wa nidhamu, wimbo unasema:

Kiongozi: *Mwana mikula pelaje kilawa.*
*Ulaganiza mhela mkahembe.*

Tafsiri

Kiongozi: *Mtoto mshenzi ukome kudamkia chumbani kwa wazazi,*
*Utajakuta kifaru mwenye pembe,*

Katika wimbo huu, vijana wanaonywa wasiwe na tabia ya kuingia chumbani kwa wazazi wao mapema asubuhi wasije wakaona mambo wasiyopaswa kuyaona. Vijana wa jamii ya Wagogo waliopata na kuyashika mafunzo ya jando huwa hawaingii kabisa kwenye vyumba vya wazazi na vya dada zao. Isitoshe, hata jikoni, hawapaswi kuingia kwa sababu ni sehemu ya wanawake. Vijana wanaoenenda kinyume na maelekezo haya walikuwa wanachukuliwa kuwa hawakufuzu mafunzo ya jando hivyo hawafai kuwa waume wala hawastahili kupewa dhamana ya uongozi katika jamii. Vilevile, wimbo huu unawafunza vijana

kuwa tendo la ndoa hufanyika mahali pa faragha, chumbani na chumba hicho kinapaswa kuheshimiwa.

Kwa upande mwingine, wimbo wa *Tati na tati cali wasagati* umebeba maudhui ya kuwataka vijana kujua mipaka baina yao na mama zao hususani kwenye masuala ya ndoa na unyumba. Wimbo unaimbwa:

Kiongozi: *Tati na tati cali wasagati,*
*Caganile nimu ikudya mbata x 2*
Wote: *Nheme itoga itoga nhegulile yaya x 2*

Tafsiri

Kiongozi: *Hapa na hapa tulikuwa wawindaji,*
*Tulikuta limnyama linakula swala x 2*
Wote: *Nikate ini nimpelekee mama x 2*

Wimbo huu unahusu vijana wawindaji waliokuta nyama akiwa anakula swala, mtunzi wa wimbo anauliza je, vijana wakate maini wampelekee mama? Maana yake ni je, wachukue hiyo habari wakamsimulie mama walichokiona porini? Wimbo huu unatumia mafumbo ambayo maana yake ni kuwasisitiza vijana kuchagua na kuchuja taarifa zipi za kusema kwa mama zao na zipi za zinawahusu wao kama wanaume. Vijana ambao ni viongozi wa baadaye wa familia na jamii hawapasi kueleza kila kitu kwa mama zao. Wanapaswa kutunza siri ya mambo mazito wanayoyaona, kuyashuhudia na kukutana nayo huko porini na katika maisha kwa jumla. Kwa kufanya hivyo, wanaonesha ukomavu wao katika kuyamudu maisha yao, ya familia na jamii kwa jumla.

Wimbo mwingine wenye maudhui kama haya, ya umuhimu wa vijana kutunza siri kuhusu masuala ya tendo la ndoa ni ule unaoitwa *Cipela cidya ne mzinzi waco.* Wimbo unasema:

Kiongozi: *Cipela cidya ne mzinzi waco,*
*Nhemunyamunya g'hema ne wanangu x 2*

Tafsiri

Kiongozi: *Kaubuyu kale na utamu wake,*
*Nilikimung'unyamung'unya peke yangu nikawanyima hata wanangu x 2*

Mwimbaji wa wimbo huu anasimulia kuhusu kaubuyu katamu alikokula akakimung'unyamung'unya peke yake akawanyima hata watoto wake. Kaubuyu kanakozungumziwa hapa ni tendo la ndoa ambapo mwimbaji alishiriki peke yake bila kuwashirikisha watoto wake. Wimbo umebeba maudhui ya kuonesha kuwa tendo la ndoa ni kwa watu wazima. Tunafahamu kuwa wazazi hupenda kuwapa

watoto wao vitu vizuri hata hivyo pamoja na utamu na uzuri wa tendo la ndoa, mzazi hawezi kuwashirikisha watoto wake. Kwa hiyo, vijana wanafundishwa kuwa kuna masuala ya kiutu uzima ambayo hayapaswi kuelezwa kwa watoto au watu wasiohusika.

Isitoshe, wimbo wa *Nyakanangali kagwa katenyanjika* umebeba maudhui ya kuonesha umuhimu wa kushirikiana baina ya mwanamume na mwanamke katika kufanikisha tendo la ndoa. Wimbo unasema:

Kiongozi: *Nyakanangali kagwa katenyanjika,*
*Nyakatongolo kambila maganza x 2*

Tafsiri

Kiongozi: *Mnangali (aina ya mti) umeanguka umelegea,*
*Faru kakinga viganja x 2*

Katika wimbo huu, aina ya mti wa mnangali umetumika kuwakilisha kiungo cha uzazi cha mwanamume. Wimbo unasema, mti umeanguka ukalegea yaani kiungo cha uzazi cha mwanamume hulegea na faru yaani mwanamke, kakinga viganja. Wimbo unasawiri suala la tendo la ndoa ambapo mwanamke anapokea kitu kutoka kwa mwanamume. Wimbo kwa hiyo, unawafundisha vijana masuala ya tendo la ndoa ambalo linapaswa kufanywa kwa ukamilifu ili mwanamume na mwanamke wote waweze kulifurahia tendo hilo kikamilifu.

Wimbo mwingine ambao una maudhui ya kuwaandaa vijana kwa ajili ya majukumu ya utu uzima unaoitwa *Mtema izengo teme lya mutumba*, unaimbwa:

Kiongozi: *Mtema izengo teme lya mutumba,*
*Lya mucengeje dimalaga hengo x 2*

Tafsiri

Kiongozi: *Mkata fito kata ya mti wa mtumba,*
*Aina ya mti wenye mibamiba humaliza panga x 2*

Wimbo huu unawaasa vijana kutokujamiina na mwanamke ambaye yupo katika hedhi. Wimbo unatumia mti wa mtumba kuonesha mwanamke ambaye hayupo katika mzunguko wa hedhi, ambaye ndiye salama kufanya naye tendo la ndoa. Kwa upande mwingine, wimbo unawatahadharisha vijana kuhusu aina ya mti wa *muchenjege* wenye miibamiiba mingi midogomidogo ambayo ni hatari maana unaharibu panga. Mti wa miibamiiba umetumika kumwakilisha mwanamke ambaye yupo katika hedhi. Wimbo unafafanua madhara ya kufanya tendo la ndoa na mwanamke ambaye yupo katika siku zake kuwa ni kumaliza panga yaani kuleta madhara ya kiafya kwa kiungo cha mwanamume. Hivyo, wimbo huu nao umebeba maudhui kuhusu majukumu ya utu uzima hususani tendo la ndoa. Kupitia wimbo

huu vijana wanapaswa kuelewa kuwa siyo wakati wote ambapo mwanamke anaweza kujamiiana kutokana na maumbile yake ya kibayolojia.

Isitoshe, wimbo wa *Kucilima kudya kuli nzoka nhiti* nao una maudhui ya kuwaandaa vijana kwa ajili ya majukumu ya ndoa na unyumba. Wimbo unasema:

Kiongozi: *Kucilima kudya kuli nzoka nhitu,*
*Ihimbaga malindi idongoye x 2*

Tafsiri

Kiongozi: *Mashariki kule kuna nyoka mweusi,*
*Anachimbaga mashimo amebinuka x 2*

Wimbo huu unawafundisha vijana namna ya kufanya tendo la ndoa kwa kutumia mtindo wa kubinuka. Nyoka mweusi anayetajwa kwenye huu wimbo, ambaye anachimbaga mashimo akiwa amebinuka ni kiungo cha uzazi cha mwanamume, wakati mashimo yanawakilisha kiungo cha uzazi cha mwanamke. Maudhui ya wimbo huu yanawapa vijana maarifa zaidi kuhusu namna ya kuyatekeleza majukumu yao ya baadaye katika ndoa. Hivyo, vijana wakiwa jandoni wanaandaliwa vema ili watakapooa waweze kutimiza vema majukumu yao ya unyumba katika ndoa zao.

Wimbo mwingine unaokaribia na huu kwa maudhui yake ni ule wa *Mgandu wetu* unaosema:

Kiongozi: *Mgandu wetu,*
Wote: *Mlagalaga msenduka,*
Kiongozi: *Kunyumba ndodo,*
Wote: *Koyali senzelesenzele msenduka x 4*

Tafsiri

Kiongozi: *Ngoma yetu,*
Wote: *Kugaragara kubinuka,*
Kiongozi: *Kwenye nyumba ndogo,*
Wote: *Kuna hekaheka za kubinuka x 4*

Wimbo huu unawafundisha vijana namna ya kufanya tendo la ndoa. Kwanza, vijana wanafundishwa kwamba hekaheka, kugaragara na kubinuka ni mambo ya kawaida wakati wa tendo la ndoa. Pili, vijana wanafundishwa kuwa tendo la ndoa hufanywa kwenye nyumba ndogo maana yake kwenye faragha. Katika jamii ya Wagogo, kwa kawaida wazazi hulala kwenye nyumba tofauti na wanayolala wanafamilia wengine. Nyumba hiyo aghalabu huwa ndogo kwa ukubwa ukilinganisha na nyingine. Lengo la kufanya hivyo ni kutunza heshima na faragha

ya tendo la ndoa. Vijana wanapaswa kufahamu kuwa tendo la ndoa halifanywi mahali popote isipokuwa mahali penye faragha na utulivu.

Pia, kuna wimbo unaoitwa *Nye mulece nisenjelece ng'hamwaje uganga nha mlango luliyaya.* Wimbo unaimbwa:

Kiongozi: *Nye mulece nisenjelece ng'hamwaje uganga nha mlango luliyaya,*
Wote: *Nye mulece nisenjelece ng'hamwaje uganga nha mlango luliyaya,*

Tafsiri
Kiongozi: *Acheni nijishunghulishe nikamwage uganga mlangoni ooh mama wee,*
Wote: *Acheni nijishunghulishe nikamwage uganga mlangoni ooh mama wee,*

Wimbo huu unawafundisha vijana kuwa watundu na kujishughulisha wakati wa kufanya tendo la ndoa, yaani wasibweteke. Maudhui ya wimbo huu yanaonesha umuhimu wa kuwa na bidii wakati wa kujamiina ili kupata matokeo mazuri. Kwa mujibu wa wimbo huu, dalili nzuri ya kuonesha kuwa tendo la ndoa limefanyika kikamilifu ni kumwaga uganga, yaani majimaji meupe yanayotoka kwa mwanamume ambayo ni ishara ya kufikia kilele cha furaha. Uganga huo humwagwa kwenye mlango, yaani kwenye sehemu za uzazi za mwanamke.

Nao wimbo wa *Cikome ca Mwamule ng'huya nene sinjise ulanga ilatonya* umebeba maudhui yanayosisitiza umuhimu wa kutumia ufundi wakati wa kufanya tendo la ndoa ili kufikia kilele cha furaha. Wimbo unasema:

Kiongozi: *Cikome ca Mwamule ng'huya nene sinjise ulanga ilatonya,*
Wote: *Cikome ca Mwamule ng'huya nene sinjise ulanga ilatonya x 2.*

Tafsiri
Kiongozi: *Kifimbo cha Mwamule (jina la mtu) ooh mimi nitikisa mbingu itanyesha,*
Wote: *Kifimbo cha Mwamule (jina la mtu) ooh mimi nitikisa mbingu itanyesha x 2.*

Katika wimbo huu kifimbo, yaani sehemu ya uzazi ya mwanamume inatakiwa kutikiswa mpaka mvua inyeshe. Mvua kunyesha imetumika kimafumbo huku ikiwa na maana ya kufikia kilele cha furaha ya tendo la ndoa. Aidha, vijana wanafundishwa kuwa tendo la ndoa siyo kwa ajili ya uzazi tu bali ni kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya mwili. Hili linajibainisha katika wimbo wa *Kabigili kabigili no mugumba nisanyanhe,* unaosema:

Kiongozi: *Kabigili kabigili no mugumba nisanyanhe,*
Wote: *Kabigili kabigili no mugumba nisanyanhe x 2*
Kiongozi: *Nisanyanhe woyeee aheee,*

Wote: *Misaaa no mugumba nisanyanhe x 4*

Tafsiri:

Kiongozi: *Kamwiba kamwiba mimi mgumba nichezecheze,*
Wote: *Kamwiba kamwiba mimi mgumba nichezecheze x 2*
Kiongozi: *Nicheze woyeee aheee,*
Wote: *Ndiye mimi mgumba nicheze x 4*

Wimbo unaeleza kuhusu mwanamke mgumba ambaye anafurahia tendo la ndoa. Kabigili ni kamwiba kagumu kagumu ambako katika wimbo huu kanawakilisha kiungo cha uzazi cha mwanamume kanamfanya mgumba achezecheze na kufurahi. Hivyo, wimbo huu una maudhui ya kumwelimisha kijana maana na umuhimu wa tendo la ndoa.

Kupitia mifano ya nyimbo hizi tunaona jinsi suala la tendo la ndoa ambalo ndilo msingi wa masuala ya uzazi linavyotiliwa mkazo katika jamii ya Wagogo. Mafundisho kuhusu ndoa yanasaidia kujenga ndoa zenye amani na upendo kwa wanandoa, familia na jamii kwa jumla. Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kwamba, mafundisho kuhusu masuala ya kiutuuzima yanatolewa kwa usiri na kwa mafumbo.

**5.3 Ujamiishaji, Uadilishaji na Malezi kwa Vijana**

Kuna nyimbo za jando kadhaa za jamii ya Wagogo ambazo zimebeba maudhui ya kuwapa maadili na mafunzo vijana ili kuwafanya wawe wanajamii wazuri kwa manufaa na maendeleo ya jamii nzima. Kwa mfano, wimbo wa *Miti yote napanda mtalawanda wani* ambao unasema:

Kiongozi: *Miti yote napanda mtalawanda wani x 2*
*Iyehe ahi yoho mtalawanda wani x 2*
*Mtalawanda wanishinda.*

Wimbo huu unamkanya kijana kutokuwa na uhusiano wa kimapenzi na dada yake au ndugu yeyote wa karibu kwa sababu ni kinyume na maadili. uhusiano wa kimapenzi na dada au ndugu wa karibu kuleta madhara kwa familia, ukoo na jamii nzima. Dada katika wimbo huu, amefananishwa na mti unaoitwa mtalawanda ambao haupandiki kutokana na matawi yake kunepa sana. Kumbi kwa hiyo, ni asasi ya ujamiishaji ambayo huwaingiza vijana katika jamii zao, huwafanya wawe wanajamii halisi kwa mawazo, hisia, mwonekano na matendo.

Nyimbo nyingine za jando zilizobeba maudhui ya kujamiisha na kuadilisha vijana ni zile zinazoimbwa wakati mwanajamii anataka kuingia kwenye *ikumbi*, yaani nyumba ya muda wanayokaa vijana waliotahiriwa na waangalizi wao. Utaratibu uliopo ni kwamba, mwanajamii haruhusiwi kuingia kwenye ikumbi bila

kupiga hodi. Kwa kawaida, mwanajamii hupiga hodi kwa kuimba wimbo, kisha wanajamii walio ndani huitikia wimbo huo ishara ya kumkaribisha. Mfano mmojawapo wa nyimbo hizi ni ule unaosema *Hodi*, unaimbwa:

Kiongozi: *Hodi,*
Wote: *Hodi karibu hodi* x 4

Wimbo huu una maudhui ya kusisitiza umuhimu wa kupiga hodi kabla ya kuingia mahali. Wimbo mwingine wenye maudhui yanayofanana na haya ni ule unaosema "*Mgulu wotama gwe yaya wotama,*" unasema:

Mpigahodi: *Mgulu watama nyeee, nyanya wotama,*
Wote: *Nyanyagule nhalanje kuli wana nyanyagule,*

Tafsiri:

Mpigahodi: *Mguu unaumaa weee, mama unaumaa,*
Wote: *Nitachechemea nikawaone watoto nitachecheme,*

Wimbo huu umebeba maudhui ya umuhimu wa kuwatembelea watu kama wagonjwa, wahitaji, wenye shida mbalimbali, ndugu, jamaa na marafiki kwa jumla. Mwimbaji anasema kwamba mguu wake unauma lakini yupo radhi achechemee ilimradi aende akawaone vijana wanavyoendelea. Hivyo, nyimbo hizi zinaeleza maadili na tabia njema ambazo vijana wanapaswa kuzifuata katika maisha yao. Kwa wimbo huu, vijana wanasisitizwa umuhimu wa kudumisha maadili mema katika jamii.

Aidha, mafunzo yanayotolewa katika jando la jamii ya Wagogo ni pamoja na malezi ya familia kwa mwanamume kama mlezi wa familia. Nyimbo za jando za Kigogo kadhaa zina maudhui ambayo yanalenga kuwaandaa vijana kwa ajili ya kuwa walezi na viongozi wa familia na jamii kwa jumla. Kwa mfano, wimbo wa *Cugulu cindya woiyeee cimemile ndeje za undeje,* ambao unaimbwa:

Kiongozi: *Cugulu cindya woiyeee cimemile ndeje za undeje x 2*
*Ndeje za undeje haleee camili uhemba zoumala x 2*

Tafsiri:

Kiongozi: *Kichuguu kile woiyeee kimejaa aina na aina za ndege x 2*
*Ndege za aina na aina hayaa tuamie wasimalize mtama x 2*

Kwa umbo lake la nje, wimbo unahusu kichuguu ambacho kimejaa ndege wa aina mbalimbali. Jamii inaaswa kuamia ndege hao wasije wakamaliza mtama. Kichuguu katika wimbo huu kinawakilisha jamii ambayo ina ndege, yaani wasichana wengi wazuri. Wimbo umebeba maudhui ya kuiasa jamii kuwalea na

kuwachunga vijana baada ya kutoka jandoni wasije wakaanzisha mahusiano na wasichana bila kufuata utaratibu unaofaa wa jamii. Wimbo huu kwa hiyo unaisawiri jamii ambayo ina jukumu hilo la malezi kwa vijana. Wimbo mwingine uliobeba maudhui ya malezi kwa vijana ni ule wa *Towe gwe*, unaimbwa:

Kiongozi: *Towe gwee,*
Wote: *Notowa nhaule wana walisungu?*

Tafsiri

Kiongozi: *Piga wewe,*
Wote: *Nitawapigaje watoto wakati wana maumivu?*

Wimbo unawaasa walezi kutowapiga au kuwapa adhabu vijana wakiwa bado wana maumivu makali ya kutahiriwa. Japokuwa, adhabu na vipigo ni muhimu katika mafunzo wakati vijana wawapo jandoni, hata hivyo, walezi wanatakiwa kusubiri mpaka maumivu yapungue. Kwa kufanya hivi, wanaonesha upendo kwa vijana ambayo ni sehemu ya malezi. Kwa ujumla, tukizingatia maudhui yaliyomo katika nyimbo hizi tunaungana na Bascom (1965) ambaye anaona kuwa fasihi simulizi, nyimbo za jando zikiwamo, ni kama Insaiklopidia ya hekima za jamii husika. Aidha, maudhui katika nyimbo hizi yanadhihirisha mawazo ya wanasosholojia ambao wanaona kuwa fasihi lazima ichukuliwe kama iliyo na uhusiano usiotatanika na maisha ya jamii (Seldon 1990). Kwa hiyo, nyimbo hizi huwakilisha maisha ya kila siku ya jamii ya Wagogo.

**5.4 Umoja, Ushirikiano na Ukarimu katika Jamii**

Nyimbo za jando za jamii ya Wagogo zina maudhui ya kusisitiza umoja na ushirikiano katika jamii. Nadharia ya Sosholojia inaamini kuwa fasihi kupitia maudhui yake ina jukumu la kujenga mahusiano kati ya mtu na mtu, mtu na kikundi cha watu au kikundi na kikundi cha watu. Wimbo wa *Kwega lete kwega lete kwega* ni mojawapo ya nyimbo zilizobeba maudhui haya, unasema:

Kiongozi: *Kwega lete kwega lete,*
Wote: *Kwega lete kwega lete kwega,*
Kiongozi: *Hamba mayowe,*
Wote: *Kwega lete kwega lete kwega,*
Kiongozi: *Hamba matama,*
Wote: *Kwega lete kwega lete kwega*

Tafsiri:

Kiongozi: *Vuta leta vuta leta,*
Wote: *Vuta leta vuta leta vuta,*
Kiongozi: *Hata karanga,*

Wote: *Vuta leta vuta leta vuta,*
Kiongozi: *Hata mahindi,*
Wote: *Vuta leta vuta leta vuta,*

Wimbo huu unawahimiza wenye nyumba kutoa chochote walichonacho na kuwapa vijana. Vitu ambavyo mara nyingi hutolewa ni kama vile mahindi, karanga, unga, mtama, pesa, na kadhalika. Maudhui ya wimbo huu ni kusisitiza ukarimu, umoja na ushirikiano katika jamii. Wanajamii wanapotoa zawadi kwa vijana wanapunguza makali kwa familia moja kulisha vijana kwa kipindi chote vijana wawapo jandoni. Ikumbukwe kwamba wakati mwingine idadi ya vijana wanaotahiriwa huwa ni kubwa kwa hiyo mahitaji ya chakula pia yanakuwa makubwa.

Wimbo mwingine unaitwa *Mwatezaga sina ndugu*. Maudhui ya wimbo huu ni umuhimu wa kuwa na ndugu. Mwimbaji kutokana na ushirikiano aliopata kutoka kwa shangazi yake, anajigamba kuwa mlisema sina ndugu, je, huyu ni nani?. Vilevile, wimbo unaoitwa *Wanyakaya nhulamusa nyee ale nhulamusa* yaani, "Wenye nyumba nawasalimia" nao una maudhui yanayodokeza umoja na ushirikiano katika jamii. Wimbo huu unaeleza kuhusu msafiri ambaye alinyeshewa na mvua katika safari yake, akafika kwenye nyumba ya watu asiowajua anasalimia na kuwaomba wamsitiri, wenyeji wanampokea vizuri na kumuuliza habari za atokako na kumpa hifadhi.

Aidha, wimbo mwingine uliobeba maudhui ya kusisitiza umoja na ushirikiano katika jamii ni ule wa *Mpela wali mubi*, unaosema:

Kiongozi: *Mpela wali mubi nyeee x 2*
*Sese causesa ne mbazo,*

Tafsiri:

Kiongozi: *Mbuyu ulikuwa mbaya weee x 2*
*Sisi ndio tuliouchonga kwa kisu*

Wimbo huu unaonesha kwamba kijana hawezi kujitahiri mwenyewe isipokuwa kwa msaada wa wanajamii wenzake. Vilevile, wimbo una majigambo ndani yake, wanajamii wanajigamba kuwa wao ndio waliouchonga mbuyu. Kwa hiyo, hapa tunaona nafasi ya watu wengine kufanikisha kitendo hicho. Kama walivyosema wahenga, mganga hajigangi na kinyozi hajionyoi, ndivyo ambavyo umoja na ushirikiano ni muhimu katika jamii.

Wimbo wa *Nye wayangu si nalikuza lwimbo lwanyemile,* nao una maudhui yanayosisitiza umoja na ushirikiano, unasema:

Kiongozi: *Nye wayaya cinalikuza,*
Wote: *Lwimbo lwanyemile x4*

Tafsiri:

Kiongozi: *Kina mama nisingekuja,*
Wote: *Wimbo umenivut x4*

Maudhui ya wimbo huu husisitiza umuhimu wa kujumuika pamoja na wengine katika masuala ya kijamii. Mwimbaji anasema kwamba hakupanga kuja lakini amevutwa na nyimbo zilizokuwa zinaimbwa kwenye *Ikumbi* akaamua kuja kujumuika na wanajamii wenzake. Kuimba nyimbo hizi kwa pamoja kunasaidia kudumisha umoja na ushirikiano katika jamii. Aidha, nyimbo hizi zinasisitiza umoja kati ya wazee na vijana, kwamba ni muhimu kwa vijana kuwaheshimu na kufuata mafundisho ya wazee wao.

**5.5 Kudumisha Mila, Desturi na Utamaduni wa Jamii**

Nyimbo za jando hubeba utamaduni na zinaakisi itikadi, mila na matarajio ya jamii au makundi ya kijamii (Kezilahabi, 1980; Mulokozi 2011). Nyimbo za jando za Wagogo zina maudhui yanayoshadidia mawazo ya wataalamu hawa. Kwa mfano, wimbo wa *Baba mtamwa nzole* unaosema:

Kiongozi: *Baba mtamwa nzole nane nhamigwe nzole,*
Wote: *Baba mtamwa nzole nane nhamigwe nzole x 2*
Kiongozi: *Nzole nzole,*
Wote: *Nane nhamigwe nzole nzole x 4*

Tafsiri:

Kiongozi: *Baba aliumwa kiungo cha siri na mimi naumwa kiungo cha siri,*
Wote: *Baba aliumwa kiungo cha siri na mimi naumwa kiungo cha siri,*
Kiongozi: *Kiungo cha uzazi,*
Wote: *Na mimi naumwa kiungo cha siri x 4.*

Wimbo huu una maudhui yanayodhihirisha kuwa suala la tohara ni sehemu ya utamaduni wa jamii. Vijana kwa kupitia wimbo huu, wanaambiwa kuwa baba zao nao walifanyiwa tohara kama walivyofanyiwa wao. Hivyo na wao wanapaswa kuwafanyia vivyo hivyo watoto wao watakaowazaa baadaye. Aidha, jando ni kipengele cha mila na desturi ambacho ni muhimu katika kutoa mafunzo yanayofaa kuendeleza maadili ya nchi na kujenga utamaduni wa taifa zima unaotokana na mila na desturi za watu wake (Kigume 2011). Hivyo, nyimbo za jando za Wagogo zinasisitiza wazazi kuwafundisha watoto kufuata utamaduni wa kabila lao. Vijana wanapaswa kufahamu kuwa, kwa kufuata utamaduni wao vema

wanaweza kuishi maisha bora na yenye furaha. Wanasosholojia wana hoja ya msingi wanaposema kwamba, si kazi rahisi kuitenga fasihi na masuala ya kijamii, kwani, fasihi simulizi ni chombo cha mabadiliko na ghala ya hekima za jamii na nyenzo kuu ya kuhifadhia hatua mbalimbali za maendeleo ya jamii husika (Bascom, 1965; Shorter, 1969; Okpewho, 1992; Mulokozi, 2017). Nyimbo za jando za jamii ya Wagogo zilizotokana na jamii haziwezi kutazamwa na kupimwa kutoka kwenye ombwe, bali historia ya mila na tamaduni, uchumi na siasa ya jamii tajwa vimezingatiwa katika ubainishaji wa maudhui katika nyimbo hizo.

**5.6 Uzingatiaji wa Masuala ya Ujinsia**

Nyimbo za jando za Wagogo zina maudhui yanayodokeza masuala ya kijinsia. Mfano mzuri ni wimbo wa *Usungu wo tamwa gwe* unaoimbwa:

Kiongozi: *Usungu wo tamwa gwe,*
Wote: *Mahiya usungu wo tamwa gwe,*
Kiongozi: *Munya mwana yalihai,*
Wote: *Mahiya usungu wo tamwa gwe,*
Kiongozi: *Shangazi munhu yalihai,*
Wote: *Mahiya usungu wo tamwa gwe,*
Kiongozi: *Yaze yasinjise iwega,*
Wote: *Mahiya usungu wo tamwa gwe.*

Tafsiri:

Kiongozi: *Uchungu unauma wee,*
Wote: *Mahiya (jina la mtu mke) uchungu unauma wee,*
Kiongozi: *Mwenye mtoto yupo wapi?*
Wote: *Mahiya uchungu unauma wee,*
Kiongozi: *Shangazi yake yupo wapi?*
Wote: *Mahiya uchungu unauma wee,*
Kiongozi: *Aje achezeshe bega,*
Wote: *Mahiya uchungu unauma wee.*

Katika wimbo huu, mwimbaji anawaomba mama na shangazi wa watoto wawabembeleze na kuwapa pole watoto kwa uchungu na maumivu waliyonayo. Kwa hiyo, wimbo unasawiri masuala ya kijinsia kwa kuonesha mgawanyo wa majukumu baina ya mwanamume na mwanamke. Jukumu la kubembeleza na kufariji watoto ni la mwanamke, yaani mama au shangazi siyo la mwanamume.

Wimbo mwingine unaodokeza masuala ya kijinsia unaitwa *Gwe nyina Mazengo gwe yaya nani yokulimila* ambao unaonesha kuwa jukumu la kulima ni la mwanamume.

Kiongozi: *Gwe nyina Mazengo gwe yaya nani yokulimila?*
*Mulume yafungwa gwe yaya nani yokulimila?*
Wote: *Gwe nyina mazengo gwe yaya nani yokulimila*
*Mulume yafungwa gwe yaya nani yokulimila x 2*
Kiongozi*:* *Nye musece nye mwambulile*
Wote: *Hoiyeee x 2*
*Cili wana wa Mazengo cili wana x 4*
Kiongozi: *Wanhu wa kuno*
Wote: *Wanhu wa kuno wakumhela ikuwo*
*Ace cikulima wene wekaye*
*Kusua ndevu wakuona sawa*
*Adi ilole adi swamulo*
*Cili wana wa Mazengo cili wana*

Tafsiri:

Kiongozi: *Wee mke wa Mazengo wee hayaa nani atakulimia?*
*Mume amefungwa jela wee hayaa nani atakulimia?*
Wote: *We mke wa Mazengo wee hayaa nani atakulimia?*
*Mume amefungwa jela wee hayaa nani atakulimia?*
Kiongozi*:* *Bora tu mcheke iyeee*
Wote: *Hoiyeee x 2*
*Tu watoto wa Mazengo x 4*
Kiongozi: *Watu wa huku,*
Wote: *Watu wa huku wanatia hasira,*
*Sisi tunalima wao wamekaa,*
*Kukuna ndevu wanaona sawa,*
*Huku kioo huku chanuo,*
*Tu watoto wa Mazengo tu watoto.*

Katika wimbo huu, wanakijiji wanamuuliza mke wa Mazengo nani atamlimia maana mumewe Mazengo amefungwa jela. Swali hili linaashiria kuwa mwanamke hawezi kulima. Majibu ya swali hili yanayotolewa na watoto wa kiume wa Mazengo yanatuthibitishia wazi kuwa jukumu la kulima ni la mwanamume siyo mwanamke. Vijana wa Mazengo wanasema wao watalima kwa ajili ya mama yao. Tena wanasema wanashangazwa na kukerwa na tabia ya baadhi ya wanaume ambao hukaa tu na kuchana nywele na kujitazama kwenye kioo badala ya kuwajibika. Katika jamii hii japokuwa wote, mwanamume na mwanamke, hushiriki katika kilimo lakini mwenye jukumu hasa la kulima ni mwanamume, mwanamke humsaidia tu mumewe.

Aidha, wimbo wa *Yaya bocele cipinde ngumile zighwale,* nao unadokeza masuala ya ujinsia, wimbo unasema:

Kiongozi: *Yaya bocele cipinde ngumile zighwale, eee zighwale,*
*Yaya zighwale zali ikumi na munana eee ne munana,*

Tafsiri:

Kiongozi: *Mama pokea mkuki nikupe njiwa, eee njiwa,*
*Mama wee njiwa zilikuwa kumi ne nane eee ne nane,*

Wimbo huu unamhusu kijana aliyekwenda kuwinda na kumletea mama yake kitoweo cha njiwa. Wimbo kwa hiyo, unaonesha kuwa jukumu la uwindaji ni la mwanamume si mwanamke.

### 5.7 Kufanya Kazi kwa Bidii, Uwajibikaji na Ujasiri

Nyimbo za jando za jamii ya Wagogo zina maudhui yanayowaandaa na kuwahimiza vijana suala la kufanya kazi kwa bidii, kuwajibika na umuhimu wa kuwa na ujasiri. Wimbo wa *Mulukolongo mulokolongo* ni mfano mmojawapo wa nyimbo zinazowaandaa vijana kuwa na ujasiri, wimbo unaimbwa:

Kiongozi: *Mulukolongo mulukolongo gwee,*
Wote: *Ahee mulokolongo x 2*
*Simba yatima mukaya,*
*Yebata ng'ombe mulukolongo*
*Ahee mulukolongo.*

Tafsiri

Kiongozi: *Kwenye kolongo kwenye kolongo wee,*
Wote: *Ahee kwenye kolongo x 2*
*Simba katua nyumbani,*
*Kakamata ng'ombe kwenye kolongo,*
*Ahee kwenye kolongo.*

Wimbo huu unawasisitiza vijana kuwa na ujasiri katika maisha kiasi cha kupambana na simba aliyeingia nyumbani na kukamata ng'ombe. Hivyo, kuwa na ujasiri ni muhimu kwa maisha yao ya baadaye.

Wimbo mwingine uliobeba maudhui ya uwajibikaji ni wimbo wa *Ngadu gweee* ambao unasema:

Kiongozi: *Ngadu gweee,*
Wote: *Nzoo nhutume nzooo,*
Kiongozi: *Kululenga,*
Wote: *Nzoo nhutume nzoo,*
Kiongozi: *Kuzingwagu,*
Wote: *Nzoo nhutume nzoo.*

Tafsiri:

| | |
|---|---|
| Kiongozi: | *Ngadu (jina la mtu) weee,* |
| Wote: | *Njoo nikutume njooo,* |
| Kiongozi: | *Kuteka maji,* |
| Wote: | *Njoo nikutume njooo,* |
| Kiongozi: | *Kukata kuni,* |
| Wote: | *Njoo nikutume njooo.* |

Wimbo huu umebeba maudhui ya umuhimu wa kufanya kazi. Mzazi anamwita mtoto wake na kuanza kumtuma kazi mbalimbali kama vile kulima shambani, kuteka maji kisimani, kukata kuni na kukamua ng'ombe maziwa. Hapa vijana wanafundishwa kuwa wawajibikaji na wasiwe wajeuri wanapotumwa kazi na wazazi, watu wazima au na mwana jamii mwingine jamii yeyote.

Vilevile, wimbo wa *Yaya bocele cipinde ngumie zigwale* nao umebeba maudhui ya kuwafundisha vijana umuhimu wa kazi na uwajibika katika familia na jamii kwa jumla, wimbo unasema:

Kiongozi:
*Yaya bocele cipinde ngumile zighwale, eee zighwale,*
*Yaya zighwale zali ikumi ne munana eee ne munana,*
*Yaya gwe ne munana cideje cindya ce mwilamba,*
*Eeee ce mwilamba, yaya gwe ce mwilamba catoa muluzi pyepyepyepyee*

Tafsiri:

Kiongozi:
*Mama pokea mkuki nikupe njiwa, eee njiwa,*
*Mama wee njiwa zilikuwa kumi na nane eee na nane,*
*Mama wee na nane kindege kile cha bwawani eee cha bwawani,*
*Mama wee cha bwawani kilipiga filimbi pyepyepyepyee (sauti ya filimbi).*

Wimbo huu unamhusu kijana ambaye alikwenda msituni kuwinda na kumletea mama yake njiwa kwa ajili ya kitoweo. Kijana anasema njiwa walikuwa kumi na nane lakini kindege cha bwawani, yaani msichana kilimpigia mluzi akampa njiwa kwa hiyo wamepungua. Wimbo unaonesha jinsi kijana anavyowajibika kuhakikisha kuna kitoweo nyumbani kwa mama yake lakini pia kwa msichana ambaye anaweza kuwa mke wake hapo baadaye.

Pia, wimbo wa *Gwe nyina mazengo gwe yaya nani yo kulimila* wenye maana *Wee mke wa Mazengo wee hayaa nani atakulimia?* unaonesha suala la uwajibikaji wa vijana kwa familia, jamii na taifa kwa jumla. Katika wimbo wa

huu, wanakijiji wanamuuliza mama Mazengo nani atamlimia maana mumewe amefungwa jela. Watoto wa Mazengo wanajibu hilo swali kwa niaba ya mama yao, wanasema kuwa wao watalima. Wimbo huu kwa hiyo, unawaandaa vijana kuwa wawajibikaji. Isitoshe, wimbo unakemea tabia ya uvivu, ambapo watoto wa Mazengo wanawashangaa wanakijiji ambao hawafanyi kazi badala yake wanakaa na kuchana nywele huku wakijiangalia kwenye vioo. Kwa jumla, nyimbo za jando za Wagogo zinafundisha juu ya wajibu wa mwanamume kwa familia na jamii.

**7.0 Hitimisho**

Maudhui yaliyomo katika nyimbo za jando za jamii ya Wagogo yanaisaidia jamii kuona umuhimu wa kuthamini ukale bila kuathiri usasa. Huenda, changamoto nyingi katika jamii ya sasa, kama vile mmomonyoko wa maadili unaotokana na ukosefu wa malezi bora kwa watoto na vijana, ukosefu wa utu na uzalendo na kadhalika, zinasababishwa na tabia ya kupuuza mambo ya kale kama vile jando na unyago. Kwa hiyo, jando na unyago ni tunu na lulu za Mwafrika, asasi za mila, desturi na utamaduni zilizobeba dhima ya ujamiishaji, hivyo, hazipaswi kuuzwa. Kupitia utafiti huu, jamii inaweza kujifunza umuhimu wa kuyaenzi mambo ya kale ili kujenga misingi ya jamii bora kwa mstakabali wa taifa letu.

Makala hii imeonesha jinsi nyimbo za jadi za jamii ya Wagogo zinavyoibua maudhui anuai. Aidha, nyimbo za jando zilizochunguzwa zinadhihirisha kuwa zimesheheni maudhui kama vile umuhimu wa tohara kwa vijana, kuwaandaa vijana kumudu majukumu ya utu uzima, ujamiishaji na uadilishaji vijana na umuhimu wa ujamiishaji na uadilishaji vijana. Mengine ni umoja, ushirikiano na ukarimu katika jamii, kudumisha mila desturi na utamaduni wa jamii, uzingatiaji wa masuala ya kijinsia, kufanya kazi kwa bidii uwajibikaji na ujasiri. Aidha, Nadharia ya Sosholoija ya Fasihi imefanikisha uandishi wa makala hii kwa kuangalia uhusiano kati ya nyimbo za jando na jamii ya Wagogo. Kwa jumla, makala hii imejihusisha na uchunguzi wa nguvu za kijamii zinavyohusiana na nguvu za kisanaa. Makala imezingatia kwamba kazi ya fasihi inadhibitiwa na miundo iliyopo katika jamii kwa kuangalia uhusiano wa wanajamii katika mienendo yao ya kila siku. Fasihi hutazamwa kama usawiri mkamilifu ambao huyasawiri maisha kwa undani na huyachunguza kwa mtazamo mpana (Coser, 1963). Kwa msingi huo, nyimbo za jando za Wagogo zimetazamwa kama zao mahsusi la jamii hiyo kwa kuzingatia historia, falsafa, mila na desturi, uchumi na siasa za jamii husika. Uchunguzi uliofanywa katika makala hii kwa hiyo, umezingatia uhusiano uliopo baina ya jamii na mienendo ya shughuli za kila siku, falsafa na mitazamo ya jamii ya Wagogo. Nadharia ya Sosholojia imemwezesha mtafiti kuzichunguza kwa kina nyimbo za jando za jamii ya Wagogo na kubaini maudhui yake kwa kuzingatia hali halisi iliyopo katika jamii.

**Marejeleo**

Bascom, W.R. (1965). "The Form of Folklore: Prose Narratives". *The Journal of American Folklore*. 78: 1-19.

Booker, M.K. (1996). *A Practical Introduction of Literary Theory and Criticism*. New York: London USA Publishers.

Coser, L. (1963). *Sociology through Literature: An Introductory Reader*. London: Englewood Cliff.

Finnegan, R. (2012). *Oral Literature in Africa*. London: London Publishers House.

Goldmann, L. (1967). "The Sociology of Literature: Status and Problems of Methods". *International Social Science Journal*. *xix*(4): 493–516.

Kauti, J.M. (2013). *Mabadiliko ya Dhamira katika Nyimbo za Makuzi ya Mwanamke wa Wayao.*Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (1980). "Ushairi na Nyimbo katika Utamaduni wetu." Katika C. K. Omari na M. V. Mvungi (Wah.), *Urithi wa Utamaduni wetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House. Kur. 119-137.

Kigume, R.A. (2011). "Jando katika Kabila la Wangindo: Utafiti wa Kitunda." Katika M.M. Mulokozi (Mh.), *Fasihi Simulizi Nyimbo za Kumbi*. Dar es Salaam: TUKI. Kur. 113–134.

Leenhardt, J. (1967). The Sociology of Literature: Some Stages in its History, in Sociology of Literary Creativity. *International Social Science Journal*. *xix*(4): 517-533.

Lukacs, G. (1962). *Preface to the Theory of the Novel*. Franklin: Merlin Press.

Madumulla, J.S. (1995). *Provebs and Saying: Theory and Practice*. Dar es Salaam: TUKI.

Mazingwa, J. (1991). *Fasihi ya Kiswahili*. Peramiho: Benedictine Publication.

Mdachi, P.L. (1991). *Wanyaturu wa Singida: Mila na Desturi zao*. Ndanda: Ndanda Mission Press.

Mhando, P. na Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonesho*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mlama, P. (1981)."Sanaa za Maonesho katika Jamii za Asili." Katika C.K. Omari na M. Mvungi (Wah.), *Urithi wa Utamaduni Wetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House. Kur. 150-171.

Mnyampala, M. (1954). *Historia, Mila na Desturi za Wagogo wa Tanganyika*. Dar es Salaam: Eagle Press.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.

Mulokozi, M.M. (1983). "Utafiti wa Fasihi Simulizi." *TUKI Makala za Semina ya Kitaifa ya Waandishi wa Habari*. III: 1-25.

Mulokozi, M.M. (1989). "Tanzu za Fasihi Simulizi." *MULIKA*. Juz. *21*: 1-24.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi Simulizi na Andishi*. Dar es Salaam: Moccony Limited.

Narizvi, S. (1982). *The Sociology of Literature of Politics*. Dar es Salaam: Edmund Burke.

Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Dar es Salaam: Phoenix Publishers Ltd.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature*. Bloomington: Indiana University Press.

Sarup, M. (1989). *An Introduction Guide to Poststructuralism and Postmodernism*. Athens: University of Georgia Press.

Simeon, K.F. (1977). *Desturi na Mila za Wapare*. Tanga: Vuga Press.

Taban, L.L. (1972). *Popular Culture of East Africa: Oral Literature*. Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Welleck, R. na Warren, A. (1949) *Theory of Literature*. London: Penguin Books.